

#MAKINIKIA Kutoka Kitabu 21 Lessons For 21st Century (Changamoto Kubwa Za Karne Ya 21 Na Jinsi Ya Kuzivuka)

Kitabu cha 21 Lessons for the 21st Century ambacho kimeandikwa na mwanahistoria Yuval Noah Harari kimeeleza kwa kina sana changamoto tunazopitia kwenye karne hii na hatua tunazopaswa kuchukua ili kuzivuka.

Karibu kwenye mafunzo ya ziada kutoka kwenye kitabu hiki, ya kutuwezesha kuwa na ufahamu zaidi na kuweza kuchukua hatua zaidi.

Katika mafunzo haya ya ziada, nakushirikisha maeneo matano muhimu ambayo changamoto hizi 21 zinazaliwa.

MOJA; CHANGAMOTO YA KITEKNOLOJIA.

Kitabu kinaeleza changamoto zote za kiteknolojia zinaanzia kwenye mambo mawili;

Moja ni ukuaji wa teknolojia ya habari (INFOTECH) ambapo sasa hivi taarifa za wengi zimekusanywa na makampuni makubwa ya kiteknolojia na hivyo kuweza kutushawishi kuchukua hatua fulani. Mifumo ya kikompyuta imeweza kukua sana kiasi cha kuweza kumjua mtu kuliko anavyojijua mwenyewe. Kama umekuwa unatumia google au facebook, utagundua mitandao hiyo inajua tabia zako kuliko wewe, hivyo inakuletea aina ya vitu unavyopendelea kufuatilia. Hii ni changamoto kubwa kama watu hatutakuwa na udhibiti wa taarifa zetu.

Mbili ni ukuaji wa teknolojia ya kibaiolojia (BIOTECH) ambapo kwa sasa taarifa za ufanyaji wa kazi wa mwili wa binadamu zimeshakusanywa sana. Kwa sasa tuna uelewa mkubwa sana wa jinsi miili yetu inafanya kazi, jinsi ubongo unavyofanya kazi na hata jinsi hisia mbalimbali zinavyoibuliwa kwenye mwili, kupitia kemikali mbalimbali ambazo mwili unazalisha.

Sasa changamoto kubwa sana itakuja pale teknolojia hizo mbili zitakapoungana, yaani INFOTECH na BIOTECH, kwa mfano kunaweza kuwepo na kadi ambayo inawekwa kwenye mwili wa binadamu, ambayo inasoma taarifa za mwili na kuzituma kwenye mfumo wa kompyuta kisha kompyuta kufanya maamuzi kwa ajili ya mtu huyo. Mfano unapokuwa na huzuni, taarifa zinatuma kwenye kompyuta kwamba una huzuni na hapo kompyuta inakuchagulia wimbo mzuri wa kusikiliza.

Kadhalika magonjwa yatakuwa rahisi kugundulika kabla dalili hazijaanza kuonekana. Magonjwa mengi huanza kwa mabadiliko madogo madogo kwenye mwili ambayo hayana dalili za nje. Uwepo wa mfumo unaokagua mwili utatoa taarifa haraka kuhusu mabadiliko hayo na hivyo kuzuia ugonjwa kabla haujaanza. Magonjwa kama saratani yataweza kuzuilika mapema.

Mfumo kama huo unaonekana ni mzuri sana, lakini una hatari moja kubwa, taarifa za jinsi mwili wako unavyoendeshwa zikifika kwenye mikono ya ambayo siyo salama, unageuka kuwa mtumwa.

Pata picha taifa linaloendeshwa na raisi ambaye ni dikteta, halafu ana nguvu ya kuwa na taarifa za wananchi wake wote, anaweza kuwafanya wajisikie vile watakavyo na hata wamtukuze na kumwona yeye ndiye mkombozi wao.

Kadhalika taarifa hizo zikifika kwenye mikono ya makampuni makubwa, yatazitemia kuhakikisha unakuwa mteja wao na kununua chochote wanachouza.

Hivyo pamoja na maendeleo haya makubwa yanayoweza kutokea kwenye sekta hizi mbili, tunapaswa kuwa na udhibiti mkubwa wa taarifa zetu ili zisitumike kutufanya watumwa au wateja wa watu wengine.

MBILI; CHANGAMOTO YA KISIASA.

Muungano wa teknolojia ya habari na teknolojia ya kibaiolojia unaleta mtikisiko kwenye maadili ya uhuru na usawa. Kwa wale ambao wana umiliki mkubwa wa taarifa za wengine wanaweza kuzitemia vibaya kwa manufaa yao binafsi. Na pia wale wanaomiliki taarifa wanakuwa tabaka la juu huku wasio na taarifa wakiwa tabaka la chini.

Suluhisho lolote la changamoto za kiteknolojia ni lazima lihusishe ushirikiano wa kimataifa, kwa sababu kampuni ye teknolojia inaweza kuwa kwenye nchi moja, lakini ikakusanya taarifa za wananchi wa nchi tofauti. Mfano Facebook ipo Marekani lakini ina watumiaji dunia nzima.

Kikwazo kikubwa kwenye utatuzi wa changamoto za kiteknolojia ni mkwamo wa kisiasa na kijamii. Nchi nyingi kwa sasa zinarudi kwenye utaifa badala ya kujenga ushirikiano wa kimataifa. Mwaka 2016 ulikuwa mwaka ambao dunia iliona mambo yasiyotegemewa kutokea. Kitendo cha Uingereza kupiga kura ya kujitoa kwenye umoja wa Ulaya na Donald Trump kushinda uraisi wa marekani iliashiria namna ambayo watu wanafikiria utaifa zaidi kuliko ushirikiano wa

kimataifa. Sera kuu ya Trump imekuwa kuifanya Amerika kuwa bora kwa kujali mambo ya Amerika na siyo ya nchi nyingine.

Ushirikiano bora wa kisiasa unahitajika ili kuweza kuzitatua changamoto hizi kubwa za kiteknolojia.

TATU; KUKATA TAMAA NA MATUMAINI.

Kutokana na changamoto kuwa nyingi na kutokutabirika, watu wengi wanaishia kukata tamaa na kuona hawana cha kufanya bali kupokea hali kama ilivyo. Lakini tunapaswa kujua kwamba uwezo wetu kama binadamu ni mkubwa na tunaweza kusimama na kuzishinda changamoto zote tunazopitia.

Ili kuweza kusimama na kuzishinda changamoto hizi, lazima kwanza tuweze kudhibiti hofu zetu, tuwe na matumaini na kuwa wanyenyekevu kwa yale tunayofanya na hata kufikiri.

Moja ya vitu vinavyotupa hofu kubwa ni ugaidi na hata uwezekano wa kuwepo kwa vita ya tatu ya dunia. Lakini ukiangalia uhalisia, utagundua hii ni hofu zaidi ya uhalisia.

Kama tulivyoona kwenye uchambuzi wa kitabu, ugaidi unauwa watu wachache sana kwa mwaka ukilinganisha na ajali au magonjwa sugu. Lakini magaidi wanajua hofu zetu ziko wapi na kuzitumia vizuri.

Mwandishi anatupa mfano wa jinsi magaidi wanavyokamilisha malengo yao kwa kutumia nguvu nyingine. Anatoa mfano kama kuna mgahawa unataka kuuvuruga lakini huna nguvu, unaweza kukamilisha hilo kwa kuweka mdudu ndani ya sikio la ngombe kisha kumweka kwenye mgahawa huo. Wakati anahangaika kumtoa mdudu kwenye sikio lake, atavunja vunja kila kitu.

Hivi ndivyo ugaidi unavyoharibu taifa, kwa kuchokoza taifa kubwa na taifa hilo kuharibu taifa jingine. Rejea mfano wa Marekani na Iraq niliutoa kwenye uchambuzi wa kitabu hiki.

Katika kuchagua mfumo bora wa kuendesha nchi hata jamii, mfumo wa kidunia (SECULARISM) unaonekana kuwa bora kuliko mfumo wa kidini (RELIGION). Mfumo wa kidunia unaendeshwa kwa misingi mikuu sita;

Msingi wa kwanza ni ukweli, mfumo wa kidunia unaongozwa na ukweli, na ukweli ni ule unaoweza kudhibitishwa na siyo tu kupokelewa na kuaminiwa kama ulivyo. Ukweli ni zao la ushahidi na utafiti na siyo imani.

Msingi wa pili ni huruma, mfumo wa kidunia unasisitiza kuwa na huruma kwa wengine, kutambua mateso ambayo wengine wanapitia na kujali zaidi. Kwa mfumo wa kidunia huibi au kuua siyo kwa sababu dini imekataza, bali kwa kuwa unajua kwa kufanya hivyo unawaumiza wengine na wewe pia.

Msingi wa tatu ni usawa, mfumo wa kidunia unasisitiza sana kwenye usawa baina ya watu na makundi mbalimbali. Kwa mfumo huu unajua wewe siyo bora kuliko wengine, bali kila mtu ana upekee wake unaomfanya awe bora.

Msingi wa nne ni uhuru, mfumo wa kidunia unampa kila mtu uhuru wa kufikiri, kuchunguza na kujaribu vitu mbalimbali. Mfumo huu unaamini kwenye haki ya mtu kuwa na uhuru wa kuwa na wasiwasi, kuuliza zaidi, kupata maoni ya upande mwingine na hata kujaribu njia mbadala.

Msingi wa tano ni ujasiri wa kupambana na mifumo kandamizi na yenye upendeleo. Pia mfumo huu unasisitiza kuwa na ujasiri wa kukubali kwamba hujui au umekosea. Mfumo huu unatufundisha tusiwe waoga na kupokea kitu kama kilivyo hata kama siyo sahihi, badala yake tukipinge.

Msingi wa sita ni majukumu, mfumo wa kidunia unampa kila mtu majukumu ya kuifanya dunia kuwa sehemu bora kwa kila mtu kuishi. Hawajitui jukumu hilo na kuwakabidhi viongozi au mtu yeyote anayeonekana ndiyo wajibu wake. Bali wanajua jukumu la kuifanya dunia kuwa bora ni la kila mtu.

Misingi hii sita kwenye maisha yako binafsi na yakawa bora sana, mara zote tafuta UKWELI, kuwa na HURUMA kwa wengine, pigania USAWA kwa wote, tumia vizuri UHURU wako na kuwa JASIRI kusimamia kilicho sahihi na usisahau kubeba MAJUKUMU yako ya kuifanya dunia kuwa sehemu bora ya kuishi.

NNE; UKWELI.

Kama unajiona umevurugwa na kuzidiwa na mambo yanavyokwenda kasi duniani, basi upo sehemu sahihi na angalau unaelewa wa namna mambo yanavyokwenda. Mifumo ya kidunia imekuwa migumu sana kwa mtu mmoja kuweza kuelewa namna mambo yanavyokwenda. Kuujua ukweli imekuwa ni changamoto kubwa kwa sababu propaganda zimekuwa nyingi mno zama hizi.

Katika zama zilizopita propaganda zilisambazwa kwa vyombo vya habari kama radio, magazeti, tv na hata vitabu. Hivyo watu wote walipata ujumbe mmoja. Lakini zama hizi propaganda zinasambazwa kwa mitandao ya kijamii, hivyo kila mtu anaweza kupata propaganda inayoendana na yeye tu. Hii ni hatari sana kwa sababu watu wanazidi kugawanywa kwenye matabaka mbalimbali.

Kwa matumizi yako ya mitandao ya kijamii, mifumo ya kompyuta ya mitandao hiyo inajua kabisa wewe unapendelea nini, uko upande upi kwa yale unayofuatilia au kushiriki. Hivyo mtu anayechagua kusambaza propaganda, anaweza kuchagua propaganda zake ziweifike watu wa aina gani.

Ni vigumu sana kuujua ukweli katika zama hizi, hasa kama unafikiri ndani ya kundi. Huwezi kuujua ukweli ukiwa ndani ya kundi. Utaujua ukweli kwa kufikiri nje ya kundi, kwa kuutafuta ukweli kwa juhudi zako.

Na kama nilivyokushirikisha kwenye uchambuzi wa kitabu, zipo njia mbili za kuupata ukweli katika zama hizi, rejea kuzijua na kuzitumia ili uweze kuupata ukweli.

TANO; UJASIRI.

Binadamu tumezoea kuishi kwa hadithi, kila zama zimekuwa na hadithi zake, zama za kifashisti hadithi ilikuwa nchi yangu ni bora kuliko nchi nyingine. Zama za kikomunisti, nchi yangu inanijali na kunipatia kila ninachotaka. Zama za huria hadithi imekuwa nchi yangu inanipa uhuru wa kuishi nitakavyo. Sasa hadithi ya huria inapotea na hakuna hadithi mpya ambayo imeshatengenezwa, je unawezaje kuyaendesha maisha yako kwa ubora bila ya hadithi ya nje?

Zipo njia tatu ambazo mwandishi ametushirikisha;

Njia ya kwanza ni kuwa tayari kubadilika, chukulia maisha yako kama mabadiliko na kila siku piga hatua kuwa bora zaidi. Usikubali leo iishie ukiwa kama jana. Kumbuka dunia inabadilika kila siku, ili maisha yako yawe bora lazima na wewe uwe unabadilika kila siku.

Njia ya pili ni kutengeneza maisha yasiyo na hadithi. Kwenye uchambuzi nimekushirikisha hadithi nne za maana ya maisha ambazo wengi wamekuwa wanaziishi lakini zote siyo sahihi. Na mwandishi anasema maisha siyo hadithi, hivyo tuache kutafuta hadithi ya kuendesha maisha yetu na badala yake tuishi maisha kwa kuyaelewa mateso. Mateso ndiyo kitu kikuu tunakutana nacho kwenye maisha, tukiyelewa tutakuwa tumeelewa maana ya maisha yetu.

Njia ya tatu ni kufanya tahajudi. Njia pekee ya kuyaelewa mateso na kujielewa sisi wenyewe siyo kwa kufuatilia maisha ya wengine, kufuatilia habari, kuzurura kwenye mitandao ya kijamii wala kujipa kila aina ya starehe tunayotaka. Njia pekee ni kujipa muda wa kuangalia namna akili na mawazo yetu yanavyokwenda. Kwa kuangalia na siyo kujaribu kudhibiti. Njia pekee ya kufanya hili ni kwa kutahajudi. Kwenye uchambuzi nimekushirikisha yahajudi

rahisi ya kufanya ili kuweza kuangalia akili yako inavyokwenda, kuyaelewa mateso na kujielewa wewe mwenyewe.

Rafiki, tunapita kipindi cha mapinduzi makubwa na maisha mapya yanakuja, ambayo yatatikisa kabisa imani zetu na hata misimamo yetu. Tunapaswa kuwa imara ili tuweze kustawi katika nyakati hizi za mapinduzi. Fanyia kazi haya uliyojifunza ili mabadiliko yanayotokea yasikuache wewe nyuma.

Uchambuzi huu wa kitabu umeandaliwa na Dr. Makirita Amani.

Dr Makirita ni daktari wa binadamu, kocha wa mafanikio, mwandishi na mjasiriamali. Kuendelea kupata chambuzi hizi za vitabu kwenye TANO ZA JUMA, hakikisha unajiunga na channel ya TANO ZA JUMA ambayo ipo kwenye mtandao wa telegram.

Kujiunga ni bure kwa juma la kwanza, kisha baada ya hapo unachagua kulipa tsh elfu moja kwa juma, au elfu tatu kwa mwezi au elfu 30 kwa mwaka. Kwa maelezo zaidi tuma ujumbe kwenda namba 0717396253, ujumbe utumwe kwa njia ya telegram pekee.

Karibu sana.